

TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa)

WITO KWA WASANII KUSHIRIKI KATIKA
TAMASHA LA 39 LA KIMATAIFA LA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO
KUANZIA TAREHE 19 HADI 26 SEPTEMBER 2020

Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo_TaSUBa (*Zamani Chuo Cha Sanaa Bagamoyo*) inapenda kuwakaribisha wasanii na vikundi vya sanaa kwa ujumla kuomba kushiriki kwa kufanya maonyesho katika Tamasha la 39 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo ambalo litafanyika katika viwanja vya taasisi (TaSUBa - Bagamoyo) kuanzia tarehe **19 hadi 26 Septemba, 2020**.

Tamasha hili limekuwa na malengo mbalimbali ikiwemo kuendeleza na kudumisha utamaduni wa Mtanzania, kubadilishana uzoefu na kujifunza kutoka kwa wasanii na vikundi vya ndani na nje ya Tanzania kupitia warsha na maonyesho mbalimbali.

Tamasha hili hujumuisha aina mbalimbali za sanaa kama vile *Ngoma, Maigizo, Muziki, Sarakasi, Mazingaombwe, Vichekesho, Filamu* pamoja na maonyesho ya sanaa za ufundi (*Exhibitions*).

TaSUBa inawakaribisha wasanii na vikundi vya sanaa kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania na nje ya nchi ili kuweza kushiriki katika tamasha hili kongwe la sanaa na utamaduni wa Mtanzania.

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 31/07/2020

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia;

Barua pepe: bagamoyofest@gmail.com au bagamoyofest@tasuba.ac.tz

Tovuti: www.tasuba.ac.tz

Simu: +255(0) 023 2440032, +255(0) 763 408 792, +255(0) 715 557 676